Lo Liyong (1972) anafafanua utamaduni kama jumla ya shughuli, kumbukumbu, matumaini na mipango ya baadaye ya jamii fulani zikiwemo pia ndoto na maono ya jamii hizo. Kwa kuzua suala la maono ya jamii na mipango yake ya baadaye, mtaalamu huyu anasisitiza kuwa jamii isiyo na utamaduni thabiti haina kesho inayoweza kujivunia.

Utamaduni unaweza pia kuelezwa kama jumla ya mambo yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake. Ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao na mambo na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha na jamii nyingine. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa utamaduni huipa jamii upekee na kuifanya kutambuliwa kwa njia maalum. Jamii yoyote inayotaka kuendelea kutambulika na kuenziwa sharti iwe na upekee katika vipengele mbalimbali vya kitamaduni. Utamaduni ni kitu kilicho hai na hivyo hutekeleza dhima maalum katika jamii. Dhima hizi ni pamoja na:

a) Kujenga na kuendeleza moyo wa kujiamini kama wananchi wa taifa moja.
b) Kuwepo na ubunifu wa vifaa, stadi, mbinu na taratibu za kufikiri na kutenda ili kudumisha uhai na kuboresha hali ya maisha ya binadamu na mazingira yake.
c) Kuwepo na utambulisho wa taifa kupitia kwa lugha, bendera ya taifa, wimbo wa taifa, vazi la taifa na nembo ya serikali.
d) Kujenga elimu bora inayoendeleza ujuzi na uzoefu unaoakisi misingi ya kimaadili inayoweza kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Tunatambua kuwa mila na desturi hujengwa, hukomaa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Iwapo jambo hili halitatekelezwa, pana hatari ya kufifia kwa utamaduni na hata kutokomea kabisa. Hatua zozote zinazoweza kuchukuliwa na serikali, watu binafsi au vikundi vya kijamii kwa lengo la kutambua na kuimarisha mila na desturi nzuri na kupinga tamaduni mbovu hazina budi kuhimizwa. Serikali na wananchi wa Jamhuri ya Kenya wametilia hili maanani na kuhakikisha kuwa linatambuliwa katika katiba. Katika Sura ya Pili, Kifungu 11 cha Katiba ya Kenya, imebainishwa kuwa:

1. Katiba hii inatambua utamaduni kama msingi wa taifa na jumla ya ustaarabu wa watu wa taifa la Kenya.
2. Serikali:-
    a) Itakuza aina zote za kitaifa na kitamaduni za kujieleza kupitia fasihi, sanaa, sherehe za kitamaduni, sayansi, mawasiliano, habari, vyombo vya habari, uchapishaji, maktaba na turathi nyingine za kitamaduni;
    b) Itatambua jukumu la sayansi na teknolojia za kiasili katika maendeleo ya nchi;
    c) Itatambua haki za kiubunifu za watu wa Kenya.

**1. Bunge litatunga sheria:-**

a) Kuhakikisha kwamba jamii zinapewa fidia au mrabaha kwa kutumiwa kwa turathi zao za kitamaduni; na
b) Kutambua na kulinda umiliki wa mbegu na mimea mbalimbali ya kiasili, sifa tofauti za kimaumbile na matumizi yake miongoni mwa jamii za Kenya.

**Jambo hili pia limesisitizwa katika Sura ya 4, Kifungu cha 44 kinachosema:**

1. Kila mtu ana haki ya kutumia lugha na kushiriki katika maisha ya kitamaduni ya chaguo lake.
2. Mtu anayetoka katika jamii ya utamaduni au lugha fulani ana haki, pamoja na wanajamii wenzake:
    a) Kufurahia utamaduni wake na kutumia lugha yake; au
    b) Kuunda, kujiunga na kudumisha vyama vya kitamaduni na kilugha na miungano mingine ya raia katika jamii.

**3. Mtu hatamlazimisha mwingine kufanya, kuzingatia au kupitia mila zozote za kitamaduni.**

Kutokana na vifungu tulivyotazama hapo juu, haki za wananchi wa Jamhuri ya Kenya zimelindwa kikatiba. Kilichobaki ni kuunda mikakati ya kuhakikisha katiba hii inatekelezwa kikamilifu kwa manufaa ya Wakenya wote. Kati ya mbinu zinazoweza kusaidia katika utekelezaji wa katiba hii, hasa kuhusiana na uenezajji wa utamaduni ni kukuza na kuzipa hadhi lugha zetu za Kiafrika, hasa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu lugha ni kitambulisho kikubwa cha wanajamii na utamaduni wao.

Kwa mujibu wa Ngugi wa Thiong'o (1986) lugha hubeba utamaduni na utamaduni hubeba amali zote ambazo hutufanya tujitambue na kupata mahali petu halisi ulimwenguni. Aidha anasisitiza kuwa tajriba za Kiafrika haziwezi kamwe kufafanuliwa kwa lugha zingine isipokuwa zile za Kiafrika. Jambo hili linazipa lugha hizi kipaumbele kama chombo cha kujiendeleza katika sekta mbalimbali, ukiwemo utamaduni.

Serikali ya Kenya, kupitia uidhinishwaji wa Katiba yake, tayari imechukua hatua ya kimaksudi ya kukikweza hadhi Kiswahili kutoka lugha ya taifa hadi lugha rasmi sambamba na Kiingereza. Lugha hii ni chombo muhimu cha kukuzia na kuenezea utamaduni wa Wakenya, hasa ikitambuliwa kuwa hii ni lugha iliyo na historia yake ndefu hapa nchini Kenya kutokana na asili yake ya Kibantu. Lugha hii pia haiwezi kamwe kudaiwa kuendeleza utamaduni wa kabila lolote nchini kwani wasemaji wake asilia si miongoni mwa zile kabila kubwa nchini.Kwa usemi mwingine, Kiswahili ndiyo lugha ya pekee inayofumbata hisia, tamaduni na matamanio ya watu wa makabila mbalimbali nchini Kenya. Aidha Kiswahili ni lugha ambayo ukubalifu wake kama lugha ya Wakenya hauwezi kutiliwa shaka

kamwe ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza ambayo ni lugha ya kigeni.

Kwa kuwa Kiswahili ni lugha inayoweza kueleweka na watu wa tabaka zote nchini, lugha hii inaweza kutumiwa kuwahamasisha wananchi ili waweze kutambua umuhimu wa vipengele muhimu vya kitamaduni vinavyoweza kuiendeleza jamii. Umma unaweza kuhamasishwa kuhusu haki ya kimsingi ya kujiunga na kushiriki kikamilifu katika vikundi mbalimbali vya kitamaduni vinavyoweza kuwaendeleza sio tu kiutamaduni bali hata kiuchumi kwa mujibu wa katiba. Fani mbalimbali za fasihi simulizi kama vile nyimbo, ngoma za kienyeji, maigizo, sanaa za maonyesho na miviga ya jamii mbalimbali, pamoja na vyombo vya habari zinaweza kutumiwa kutekeleza wajibu huu. Aidha, inaweza kutumiwa kufafanulia haki za wasanii, (watunzi, waandishi, wachapishaji na wasanii wote) ambazo zinalindwa na katiba.

Akizungumzia umuhimu wa sanaa katika uendelezaji wa fasihi simulizi ya Kiafrika, Achebe (1990) anasema kuwa sanaa imekuwa, na inaendelea kuwa chombo cha kumhudumia mwanadamu. Anaongeza kuwa sanaa sharti iwe na ujumbe na iwe na lengo fulani ili iweze kumtumikia mwanadamu. Ni kutokana na dhima hii ambapo sanaa iliyomo katika lugha ya Kiswahili inaweza kutumiwa kuhubiri amani miongoni mwa vikundi mbalimbali vya kijamii, hasa wakati wa michezo na tamasha nyingine za kitamaduni, hususan zile zinazojumuisha watu wa makabila mbalimbali. Jambo hili tayari limefaulu pakubwa katika kuunganisha jamii za Wapokot na Waturkana kupitia juhudi za mwanariadha maarufu Tegla Loroupe.

Wakati wa tamasha za aina hii, umuhimu wa michezo katika kujenga mwili, afya, akili, nidhamu, ushirikiano na uhusiano baina ya watu binafsi, makundi, maeneo na hata mataifa unaweza kuhimizwa. Mawasilisho mbalimbali yakiwemo mashairi, nyimbo, maigizo, semi, vichekesho na malumbano ya utani ni mbinu muhimu za kiubunifu zinazoweza kutumika kutekeleza wajibu huu. Kupitia ubunifu huu, baadhi ya sifa chanya na zile hasi za tamaduni za jamii mbalimbali pamoja na athari zake kwa jamii husika zinaweza kuzungumziwa. Kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya wananchi wote, inaweza kuwa chombo imara cha kuwaunganisha Wakenya kupitia ujumbe wa amani, ushirikiano na msamaha, hasa baada ya misukosuko ya kisiasa na kijamii iliyoshuhudiwa miaka kadha iliyopita. Kumbukumbu za historia ya Jamhuri pamoja na zile za shughuli za jamii mbalimbali nchini pia zinaweza kuhifadhiwa kwa lugha ya Kiswahili ili ziweze kuvifikia vizazi vijavyo kwa lugha yenye mnato na mguso wa Kiafrika.

Licha ya mazuri tuliyoyajadili kuhusu utamaduni, hatuwezi kupuuza athari mbaya zinazoweza kutokana na baadhi ya mila na desturi zilizopitwa na wakati. Mifano ya tamaduni mbovu ni kama: ukeketaji wa wanawake; ndoa za lazima na ubidhaaishaji wa taasisi ya ndoa; ubaguzi kwa misingi ya kijinsia, kisiasa, kidini, kiuchumi na kikabila. Katiba ya Kenya imeweka jambo hili dhahiri katika Sura ya Nne, Kifungu cha 44 (3) kuwa mtu hatamlazimisha mwingine kufanya, kuzingatia au kupitia mila zozote za kitamaduni na hivyo ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa haki za Wakenya za kuchagua, kuzingatia na kuendeleza utamaduni ufaao hazikiukwi na mtu yeyote. Hili litawezekana kupitia kuwepo kwa sera mahsusi ya kusimamia masuala ya utamaduni nchini. Kama tulivyoona hapo awali, Kiswahili bila shaka ni chombo kinachotosheleza mahitaji ya kuwafikishia Wakenya ujumbe muhimu kuhusiana na athari za tamaduni za aina hii.

**1.2 Sera ya Kitamaduni**

Licha ya kuwepo kwa ari ya kuitekeleza Katiba ya Kenya, upo umuhimu wa kutambua kuwa utekelezaji huu hauwezi kufanywa kiholela bali unahitaji kupangiwa vyema. Serikali ya Kenya haina budi kuunda sera ya kitamaduni itakayoliwezesha taifa kutumia kikamilifu fani zote za kitamaduni, kujenga na kutathmini maendeleo ya maisha ya Wakenya. Kutokana na ushirikiano wa mataifa ya Afrika Mashariki, tunaweza kujifunza kutoka kwa sera ya kitamaduni ya Jamhuri ya Tanzania inayolenga kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kueleza dhima na malengo ya utamaduni
(ii) Kubainisha jinsi shughuli za utamaduni zitakavyoendeshwa na kusimamiwa
(iii) Kueleza nafasi ya lugha ya Kiswahili, zile za kiasili na za kigeni katika taifa
(iv) Kusisitiza umuhimu wa kuhifadhi na kuendeleza urithi wa Utamaduni kupitia burudani, michezo, malezi, elimu na mafunzo
(v) Kufafanua jinsi umma utakavyoshirikishwa katika shughuli za kitamaduni
(vi) Kuweka taratibu mahsusi za kugharamia uendeshaji wa shughuli za utamaduni.

Utekelezwaji huu unaweza kutendwa kupitia wizara zinazohusika na haki na masuala ya kikatiba, utamaduni na turathi za kitaifa na vijana na michezo. Wizara ya Fedha pia haina budi kutenga fedha za kugharamia shughuli za kitamaduni nchini kwani utekelezwaji wowote lazima uwe na mahitaji ya kifedha.

**1.3 Mazingira**

Kimsingi, mazingira yanaweza kuelezwa kama hali, mambo au vitu vinavyomzunguka kiumbe mahali anapoishi au maisha yake. Hivi ni pamoja na watu, hewa, wanyama, mimea, ardhi, maji, na vitu vyote vilivyo katika uso wa ulimwengu; viwe vinaonekana au havionekani. Ni muhimu kutambua kuwa juhudi za binadamu zinaweza kuhifadhi mazingira yake au kuyavuruga na kuyafanya maisha yake kuwa magumu na ya kutamausha. Ujenzi wa mazingira huchukua

muda mrefu lakini ubomoaji wake huchukua muda mfupi tu. Mazingira yaliyoharibiwa na kuchafuliwa yanaweza kusababisha majanga makuu. Haya ni pamoja na upungufu wa mvua, na hivyo kusababisha kiangazi na njaa, ukosefu wa maji ya kutumiwa na watu na wanyama na pia viwandani, na hata kuenea kwa jangwa. Hatua za dharura zisipochukuliwa ili kurekebisha hali hii huenda pakatokea vifo vya wanyama na pia binadamu.

Katika juhudi za kuepukana na madhara haya, katiba ya Kenya imeweka bayana umuhimu wa kushiriki katika uhifadhi wa mazingira, iwe ni katika kiwango cha mtu binafsi, makundi au mashirika au vyombo vya umma. Katika Sura ya Nne Kifungu cha 42, Katiba ya Kenya inakariri kuwa:

**Kila mtu ana haki ya kuishi katika mazingira safi na salama, ambapo ni pamoja na haki ya:**

a) Kutunziwa mazingira kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo kupitia kwa hatua za kisheria na nyinginezo hasa zile ambazo zinakusudiwa katika Kifungu cha 69;
b) Kuhakikisha kuwa wajibu unaohusu mazingira, ulio chini ya kifungu cha 70 umetimizwa.

Vifungu vya 69 na 70 vya Sura ya Tano vinazungumzia kanuni na wajibu kuhusiana na mazingira. Vifungu hivi vinamhakikishia mwananchi kuwa serikali itahakikisha kuna utumiaji na uhifadhi wa rasilimali zote kwa njia zifaazo ili kuwepo ugawanyaji mwafaka wa faida zitokanazo na rasilimali hizo. Umuhimu wa kila mwananchi wa kushirikiana na serikali ili kuhakikisha haya yametimizwa pia umesisitizwa. Kifungu cha 69 kinakariri kuwa:
Serikali:

a) Itahakikisha matumizi, usimamizi na uhifadhi wa mazingira na maliasili unaodumishwa na kuhakikisha usawa katika ugavi wa faida zinazopatikana;
b) Itafanya juhudi ili kutimiza na kuhakikisha kuwa angalau asilimia kumi ya ardhi ya Kenya imepandwa miti;
c) Italinda na kukuza hakimiliki za rasilmali za kiakili na elimu ya jadi ya uanuwai wa viumbe na rasilmali za kinasaba za kuzaliwa za kijamii;
d) Itahimiza kushiriki kwa umma katika usimamizi, utunzaji na uhifadhi wa mazingira;
e) Italinda rasilmali zote za kinasaba na uanuwai wa kielimu viumbe;
f) Itaanzisha mifumo ya kutathmini athari za mazingira, ukaguzi wa mazingira na usimamizi wa mazingira hayo;
g) Itatupilia mbali michakato na shughuli ambazo zinaweza kuhatarisha mazingira; na
h) Kutumia mazingira na maliasili kwa manufaa ya Wakenya.

Kifungu hiki pia kinasisitiza wajibu wa kila mtu wa kushirikiana na idara za serikali na watu wengine katika kulinda na kuhifadhi mazingira na kuhakikisha kuna maendeleo ya kiekolojia na matumizi ya rasilmali.

Mapendekezo haya yataweza tu kuwa na maana na manufaa kwa mwananchi wa kawaida iwapo tafsiri yake itatolewa kwa lugha ya Kiafrika inayoweza kumjengea taswira kamili ya kinachozungumziwa. Hii ni kwa sababu masuala ya mazingira aghalabu hufafanuliwa kwa lugha za kigeni, hasa Kiingereza kupitia matumizi ya istilahi ngumu za kisayansi ambazo ni ngumu kung'amuliwa na watu wasio na ufahamu wa juu wa masuala haya.

Lugha ya Kiswahili inaweza kuwa chombo imara cha kuelimishia umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira, faida tunazopata kutokana nayo na hasara zinazotokana na uharibifu wa mazingira. Iwapo hili litatekelezwa kikamilifu, hali ya swintafahamu kama iliyozuka kuhusiana na uvamizi wa misitu mbalimbali humu nchini huenda isitokee tena. Juhudi za wanamazingira kama vile marehemu Wangari Maathai zinaweza kufaulu zaidi iwapo mbinu kama zile tulizojadili kuhusiana na uhifadhi wa utamaduni zitatumiwa kueneza ujumbe kuhusiana na uhifadhi wa mazingira.

Matangazo kuhusiana na masuala mbalimbali ya kimazingira pia yanaweza kutolewa kwa Kiswahili kupitia maandishi na michoro kwenye mavazi kama vile leso, vitenge, shati, shuka na hata blanketi. Wachapishaji wa vitabu pia wanaweza kuhimizwa kuweka ujumbe kama huu kwenye jalada za vitabu vinavyotumika katika viwango mbalimbali ili kusisitiza suala hili. Aidha, tafsiri za kazi mbalimbali kuhusiana na mazingira zilizoandikwa kwa lugha za kigeni zinaweza kufanywa kwa Kiswahili na kuchangia pakubwa katika juhudi za uhifadhi wa mazingira. Hili litahakikisha kuwa Wakenya wana nafasi bora ya kuelimishwa kuhusu mazingira na hivyo kupuuza uharibifu unaosababishwa na kutojua.

Lugha hii pia itawazindua wananchi juu ya haki zao kuhusiana na utumiaji wa rasilmali za kimazingira zilizonakiliwa katika Kifungu cha 70 cha Sura ya Tano. Haki hizi ni pamoja na:

(i) Kuzuia, kukomesha au kuachisha tendo au kosa lolote hatari kwa mazingira;
(ii) Kumshurutisha afisa yeyote wa umma kuchukua hatua ya kuzuia au kukomesha tendo au kosa lolote hatari kwa mazingira; ama
(iii) Kutoa fidia kwa mwathiriwa yeyote anayeathirika kutokana na ukiukaji wowote wa haki ya kupata mazingira safi na salama kiafya.

Iwapo wananchi watapata mwamko kamili na kupinga kabisa uharibifu wa mazingira, ni dhahiri kuwa Kenya itakuwa Paradiso duniani.

**1.4 Hitimisho na Mapendekezo**

Katika makala haya tumeona umuhimu wa uhifadhi wa utamaduni pamoja na mazingira yetu. Tumeona pia mikakati mbalimbali inayoweza kupangwa, kuhimizwa na pia kutekelezwa katika juhudi hizi muhimu. Nafasi ya Kiswahili katika kuwezesha kukamilika kwa juhudi hizi pia imejadiliwa. Pia tumeona jinsi serikali ya Jamhuri ya Kenya inatambua juhudi hizi na kuzitia maanani kupitia utengaji wa nafasi katika stakabadhi hii muhimu na pia kuwapa wananchi nafasi ya kutoa maoni yao kama haki yao ya kikatiba. Kilichobaki sasa ni utekelezaji wa sheria hizi na kuhakikisha kuwa hazikiukwi hata kidogo. Serikali pekee haiwezi kamwe kutekeleza Katiba - kila Mkenya sharti awajibike. Hatuna budi pia kukuza na kuimarisha utamaduni unaotutambulisha kama Wakenya wala si vikundi vya kikabila na pia kupinga kwa nguvu zote ubugiaji wa mila na desturi za kigeni zinazoweza kutupotosha kwani mwacha mila ni mtumwa.

Kwa kuwa Katiba inahimiza kutambua na kulinda umiliki wa mbegu na mimea ya kiasili, matumizi yake miongoni mwa wanajamii pamoja na jukumu la sayansi na teknolojia za kiasili katika maendeleo ya nchi, hatuna budi kudhibiti matumizi ya rasilmali hii muhimu. Miaka michache iliyopita, tulishuhudia Wakenya na walimwengu wengine, hasa kutoka nchi za Afrika Mashariki wakifunga safari hadi kijiji cha Loliondo, Tanzania, kutafuta msaada kutoka kwa mzee Ambilikile Mwasapile aliyeaminika kuwa na tiba ya maradhi ainati.

Kuna haja ya kuwashirikisha kikamilifu na kwa uangalifu watu walio na ujuzi kuhusiana na dawa zitokanazo na mazingira yetu katika utafiti wa kuaminika ili mazingira yetu yachangie kikamilifu katika uhifadhi wa afya zetu. Uhifadhi na upanzi wa miti na mimea mingine ya kiasili pia hauna budi kuhimizwa ili rasilmali hii muhimu isiangamizwe na watu wachache walio na maarifa na ujanja wa kuitumia kujinufaisha kiuchumi. Lugha ya Kiswahili haina budi kutumiwa katika kuuelimisha umma ambao unaweza kudanganyika kwa urahisi na kuhatarisha afya na maisha yake.

**MAREJELEO**

1. Achebe, C. (1990). Hopes and Impedimemts: Selected Essays. New York: Anchor Doublesday.
2. Fowler, D. (1987). Katika Giglioli, P. (Ed.) Language and the Social Context. Middlesex: Penguin.
3. Lo Liyong, T. (1972). Preface to the Popular Culture of East Africa. Nairobi: Longman.
4. Mazrui, A. (1985). Swahili, State and Society. Nairobi: East African Education Publishers.
5. The Constitution of Kenya, 2010 – Kenya Law Reform Commission. http://www.klrc.go.ke. Imepakuliwa 19.07.03
6. TUKI (2004) Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Oxford University Press.
7. Wa Thiong'o, N. (1986) Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature. Nairobi: Heinemann.
8. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, https://www.tanzania.go.tz. Imepakuliwa19.06.01